# BENKI KUU YA TANZANIA

# TATHMINI YA MWENENDO WA UCHUMI

Februari 2025

Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia ........ 1

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa ........ 3

2.1 Mfumuko wa Bei ........ **Error! Bookmark not defined.**

2.2 Sera ya Fedha ........ 5

2.3 Viwango vya Riba ........ 7

2.4 Masoko ya Fedha ........ 8

2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ........ 9

2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa ........ 10

2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje ........ 12

VIAMBATISHO ........ 19

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliendelea kuwa imara kwa kipindi Januari 2026, ukichochewa na kuongezeka kwa matumizi binafsi, uwekezaji endelevu wa kiteknologia, na masharti nafuu ya kifedha ambapo kwa pamoja vimechangia kupunguza athari za migogoro ya siasa za kijiografia na kiabiashara (Kielelezo 1.1a na Kielelezo 1.1b). Mwenendo wa shughuli za kiuchumi katika nchi zilizoendelea uliendelea kuimarika, sambamba na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji viwandani. Kasi ya ukuaji katika nchi zinazoibukia kiuchumi iliendelea kuwa na mwelekeo mchanganyiko[1]. Nchini China, mahitaji ya ndani yalibaki kuwa dhaifu , japokuwa hatua za sera mahsusi ulileta nafuu. Uchumi wa India uliendelea kuwa imara, ukichochewa na huduma pamoja na uwekezaji. Barani Africa, Kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi uliendelea kuwa himilivu licha ya masharti magumu ya upatikanaji wa fedha kutoka nje na kuongezeka kwa hali ya kutotabirika kwa hali ya siasa za kijiografia na biashara duniani.

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Biashara Duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

Kwa ujumla, bei za bidhaa mbalimbali duniani zilikuwa zenye mwelekeo wa kuongezeka katika kipindi cha mwezi Januari 2026 (Kielelezo 1.2). Bei ya mafuta ghafi zilipanda ikiakisi kuongezeka kwa mvutano wa siasa za kijiografia, hususan baina ya Marekani na Iran. Bei ya dhahabu iliendelea kuongezeka katika masoko makuu, ikichochewa na ongezeko la mahitaji makubwa ya mali salama katika masoko makuu na ununuzi unaoendelea wa benki kuu.

Licha ya mahitaji makubwa duniani, bei ya kahawa aina ya Arabika ilishuka kidogo, kwa

[1] Global economic prospects January 2026

sehemu ikichangiwa na matarajio ya ongezeko la mavuno nchini Brazil na kuongezeka kwa matumizi ya kahawa ya bei nafuu aina ya Robusta, ambayo ilisaidiwa na usambazaji wa kutosha, hasa kutoka Asia. Bei za mafuta ya mawese ilipanda ikichangiwa na uhitaji mkubwa na kupungua kwa uzalishaji wa msimu nchini Malaysia na Indonesia. Vilevele, bei ya ngano iliongezeka kutokana na hali mbaya ya hewa, iliyoathiri uzalishaji nchini Urusi na Marekani. Bei ya mbolea (Urea na DAP) ilionyesha mwelekeo mchanganyiko: bei ya Urea ilipanda kwa kiasi kikubwa kutokana na gharama kubwa za malighafi, hususan gesi asilia, huku bei ya DAP ikishuka kutokana na mahitaji hafifu. Bei ya sukari ilishuka kutokana na uzalishaji mkubwa, hali inayoashiria uwepo wa ziada kubwa ya bidhaa hiyo duniani (Kiambatanisho, Jedwali A8).

Kutokana na mabadiliko ya bei za bidhaa, kasi ya mfumuko wa bei duniani uliendelea kupungua, ikichochewa na kupungua kwa shinikizo la uhitaji. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei ulipungua zaidi ukikaribia malengo ya sera ya fedha. Miongoni mwa nchi zinazoibuka kiuchumi, China iliendelea kuwa na mfumuko mdogo wa bei, huku India ikishuhudia ongezeka. Katika Africa, Kusini mwa Jangwa la Sahara, hususani ndani ya kanda za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), mfumuko wa bei ulibaki ndani ya viwango vya ulinganifu vya mtangamano, vikichangiwa na udhabiti wa bei za vyakula na kupungua kwa mfumuko wa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje (Kielelezo 1.3, Kielelezo 1.4 na Kielelezo 1.5).

**Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




Chanzo: Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects
Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazochipukia Kiuchumi**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei Kwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**




Chanzo: Ofisi za Taifa za Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei kwa mwezi Januari 2026 uliendelea kuwa ndani ya wigo wa kitaifa wa asilimia 3 hadi 5, sambamba na vigezo vya utangamano wa SADC na EAC. Mfumuko wa bei ulipungua kufikia asilimia 3.3 kutoka asilimia 3.6 mwezi Desember 2025, juu kidogo ya asilimia 3.1 iliyorekodiwa mwezi Januari 2025 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.1). Hali hii ilitokana na kupungua kwa mchango wa mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi na kuendelea kupungua kwa mfumuko wa bei wa vyakula visivyochakatwa (Kielelezo 2.1.3).

Mfumuko wa bei wa chakula ulishuka hadi kufikia asilimia 5.7 mwezi Januari 2026, kutoka asilimia 6.7 mwezi Desemba mwaka 2025, juu ya asilimia 5.3 mwezi Januari 2025. Kupungua kwa mfumuko wa bei wa chakula katika kipindi cha mwezi Januari 2026 kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na utulivu wa bei za baadhi ya mazao ya vyakula vikuu na mbadala, hususan ulezi, mtama na maharage (Kielelezo 2.1.4a na Kielelezo 2.1.4b).

**Jedwali 2.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

| | | Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiliko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Jan-25 | Des-25 | Jan-25 | Jan-25 | Des-25 | Jan-25 |
| Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 1.2 | 2.0 | 0.3 | 5.3 | 6.7 | 5.7 |
| Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 1.4 | 0.4 | 0.2 | 3.6 | 3.4 | 2.2 |
| Nguo, Mavazi na Viatu | 10.8 | 0.8 | 0.2 | 0.0 | 1.9 | 2.0 | 1.2 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | 0.2 | 0.5 | 0.2 | 2.2 | 2.3 | 2.3 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 0.3 | 0.2 | 0.0 | 2.2 | 3.0 | 2.7 |
| Afya | 2.5 | 0.3 | 0.1 | 0.1 | 1.4 | 1.3 | 1.1 |
| Usafiri | 14.1 | 0.0 | 1.4 | 0.2 | 2.4 | 4.1 | 4.2 |
| Habari na Mawasiliano | 5.4 | -0.1 | 0.2 | 0.2 | 0.8 | 0.5 | 0.9 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 0.3 | -0.1 | 0.6 | 1.7 | 0.3 | 0.6 |
| Elimu | 2.0 | 2.9 | 0.0 | 0.3 | 4.5 | 2.9 | 0.4 |
| Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 0.1 | 0.0 | 0.3 | 1.7 | 0.9 | 1.1 |
| Bima na Huduma za Kifedha | 2.1 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.8 | 0.4 | 0.5 |
| Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 0.9 | -0.3 | 2.9 | 3.1 | 1.2 | 3.2 |
| Fahirisi Bidhaa Zote | 100.0 | 0.6 | 0.9 | 0.2 | 3.1 | 3.6 | 3.3 |
| Makundi Mengine Teule | | | | | | | |
| Faharisi ya Bidhaa za Msingi | 73.9 | 0.5 | 0.4 | 0.2 | 2.7 | 2.5 | 2.2 |
| Fahirisi Isiyojumuisha Fahirishi za Bidhaa za Msingi | 26.1 | 1.0 | 2.2 | 0.4 | 4.0 | 6.7 | 6.0 |
| Fahirisi za Mafuta, Nishati na Bili za Maji | 5.7 | -0.1 | 1.3 | -0.1 | 3.5 | 4.6 | 5.2 |
| Fahirisi za Huduma | 37.2 | 0.3 | 0.5 | 0.3 | 1.0 | 2.0 | 4.6 |
| Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 0.8 | 1.2 | 0.2 | 4.2 | 4.5 | 2.1 |
| Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 2.0 | -0.1 | 0.3 | 4.0 | 2.2 | 3.9 |
| Fahirisi za Bidhaa zote Isipokuwa Chaakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi | 71.8 | 0.3 | 0.5 | 0.2 | 2.1 | 2.3 | 2.2 |

Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.1: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili**




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.2: Mfumuko wa Bei na Malengo Yake.**

asilimia




Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.3: Mchango Katika Mfumuko wa Bei**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.4: Kiwango cha Mfumuko wa Bei za Mazao**

**a. Mazao ya Vyakula Vikuu**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**b. Mazao ya Vyakula Mbadala**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya chakula kinachohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) nchini ilipungua hadi tani 567,469 mwezi Januari 2026 kutoka tani 577,376 mwezi Desemba 2025.Kupungua huku kulitokana na uuzaji wa tani 9,907 za mahindi na mpunga kwa wafanyabiashara (Jedwali 2.1.2).

**Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 | 567,469 |
| Feb | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 | |
| Mac | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 | |
| Apr | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 | |
| Mei | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 | |
| Jun | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 | |
| Jul | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 | |
| Ago | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 | |
| Sep | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 | |
| Okt | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 | |
| Nov | 147,401 | 244,223 | 702,502 | 590,425 | |
| Des | 137,655 | 248,282 | 677,115 | 577,376 | |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi ulipungua hadi asilimia 2.2 mwezi Januari 2026 kutoka asilimia 2.7 mwezi kama huo mwaka 2025, kutokana na kupungua kwa bei za mavazi, viatu, samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati (Kielelezo 2.1.1 na Jedwali 2.1.1).

Mfumuko wa bei wa nishati, mafuta na bili za maji uliongezeka hadi asilimia 5.2 Januari 2026, kutoka asilimia 3.5 mwezi kama huo mwaka 2025 (Kielelezo 2.1.5 na Kielelezo 2.1.1). Mwenendo huu umetokana na kuongezeka kwa gharama za kuni na mkaa.

**Kielelezo 2.1.5: Bei za Bidhaa za Mafuta**

TZS kwa Lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## 2.2 Sera ya Fedha

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC), katika kikao chake kilichofanyika mwezi Januari 2026, iliamua riba ya Benki Kuu (CBR) kuendelea kuwa asilimia 5.75 kwa robo ya mwaka unayoishia Machi 2026. Uamuzi huo ulitokana na matarajio ya mfumuko wa bei kubaki ndani ya wigo wa kitaifa wa asilimia 3–5. Sanjari na mwelekeo huu, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/-2, sambamba na riba ya Benki Kuu.

Utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwezi Januari 2026 ulikuwa wa kuridhisha, hivyo kuchangia uwepo kwa ukwasi wakutosha kwenye mabenki . Kufuatia mwenendo huu, riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki iliendelea kuwa karibu na kiwango cha riba ya Benki Kuu (Kielelezo 2.2.1). Aidha, uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi wa shilingi ulipunguza utegemezi wa mabenki kwa nyenzo za kuongeza ukwasi kutoka Benki Kuu, kama inavyoakisiwa kwa kupungua kwa miamala ya mikopo ya muda mfupi kwa mabenki (reverse repo). Mikopo kwa mabanki kuptia *reverse repo*ilipungua kutoka shilingi bilioni 1,419.3 mwezi uliopita hadi shilingi bilioni 976.4 (Kielelezo 2.2.2).

**Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi, sambamba na mwelekeo wa sera ya fedha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 26.3 mwezi Januari 2026, ikilinganishwa na asilimia 25.8 Desemba 2025 , ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1). Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 23.5, karibu sawa na ukuaji uliorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.2.4 na Kielelezo 2.2.5).

**Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake**

| | Kiasi (Shilingi Billioni) | | | Ukuaji kwa mwaka (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipengele** | Jan-25 | Des-25 | Jan-26 | Jan-25 | Des-25 | Jan-26 |
| Rasilimali halisi za nje | 12,688.5 | 15,283.5 | 15,950.0 | 22.3 | 12.7 | 25.7 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 10,927.2 | 13,707.3 | 13,987.7 | -3.0 | 15.5 | 28.0 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 1,761.4 | 1,576.1 | 1,962.3 | --- | --- | 11.4 |
| Rasilimali halisi za ndani | 37,146.0 | 46,240.8 | 46,995.3 | 11.3 | 30.8 | 26.5 |
| Madai rasmi ya ndani | 49,255.1 | 57,160.1 | 58,114.7 | 10.9 | 20.2 | 18.0 |
| Amana za Serikali zilizopo Ben | 8,046.1 | 9,607.6 | 9,705.7 | -4.4 | 18.7 | 20.6 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 36,576.1 | 44,584.6 | 45,171.4 | 12.8 | 23.5 | 23.5 |
| Rasilimali nyinginezo | -12,109.2 | -10,919.3 | -11,119.4 | 9.7 | -10.6 | -8.2 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 49,834.5 | 61,524.3 | 62,945.3 | 13.9 | 25.8 | 26.3 |
| Amana za fedha za kigeni | 12,419.3 | 13,381.1 | 14,226.8 | 24.3 | 13.7 | 14.6 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 37,415.2 | 48,143.2 | 48,718.5 | 10.8 | 29.6 | 30.2 |
| Amana zinginezo | 14,342.2 | 17,944.2 | 18,421.7 | 8.0 | 26.1 | 28.4 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 23,073.0 | 30,199.0 | 30,296.8 | 12.6 | 31.8 | 31.3 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 6,997.7 | 8,492.3 | 8,102.1 | 14.6 | 15.5 | 15.8 |
| Amana za hundi | 16,075.4 | 21,706.7 | 22,194.7 | 11.7 | 39.6 | 38.1 |
| Fedha za msingi (M0) | 11,670.3 | 14,508.3 | 15,225.1 | 12.1 | 20.7 | 30.5 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.3.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Mikopo katika shughuli za uchimbaji madini na mawe ilirekodi kiwango cha juu cha ukuaji wa mikop,o ikiongezeka kwa asilimia 91.4, ikifuatiwa na shughuli za biashara; na usafirishaji na mawasiliano ambazo zilikua kwa asilimia 50 na 34.2, mtawalia (Jedwali 2.2.2). Ongezeko la ukuaji wa mikopo katika shughuli za uchimbaji madini na mawe ulichangiwa na hatua za Serikali kuboresha sekta ya madini na kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo kwa kutumia dhamana zinazoendana na mahitaji. Kwa upande mwingine , ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za viwanda ulipungua kwa mwezi wa pili mfululizo, hali iliyochangiwa na ongezeko la marejesho ya mikopo.

Mikopo kwa shughuli binafsi ambayo kwa kiwango kikubwa hutumika kugharamia shughuli za wajasiriliamali wadogo sana, wadogo, na wakati, iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote ya sekta binafsi kwa asilimia 35.6, ikifuatiwa na biashara (asilimia 14.9) na kilimo (asilimia 13.1) (Kielelezo 2.2.6).

**Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi**

Asilimia

| | Jan-25 | Mac-25 | Jun-25 | Sep-25 | Des-25 | Jan-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini | -30.6 | -24.8 | 20.8 | 32.4 | 91.1 | 91.4 |
| Biashara | 5.0 | 12.7 | 21.3 | 24.8 | 49.7 | 50.0 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 41.6 | 36.3 | 30.2 | 27.6 | 28.9 | 34.2 |
| Ujenzi | 19.0 | 35.1 | 25.7 | 15.7 | 25.6 | 29.5 |
| Kilimo | 14.8 | 22.4 | 25.7 | 17.4 | 29.4 | 27.9 |
| Shughuli binafsi | 1.3 | 5.4 | 22.5 | 16.3 | 2.5 | 17.8 |
| Hoteli na migahawa | 13.9 | 9.4 | 13.7 | 14.7 | 17.7 | 1.6 |
| Viwanda | 18.0 | 10.9 | 2.5 | 0.1 | -8.2 | -7.7 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

**Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi**

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.3 Viwango vya Riba

Kwa ujumla, viwango vya riba katika mabenki vilikuwa tulivu kwa mwezi Januari 2026. Wastani wa riba za mikopo (overall lending rate) ulipungua hadi asilimia 15.07 kutoka asilimia 15.24 mwezi Desemba 2025, huku riba za mikopo kwa wateja wakubwa (*negotiated lending rates*) zilipungua hadi asilimia 12.25 kutoka asilimia 12.38. Wastani wa riba za amana (*overall time deposit rate*) ulikuwa asilimia 8.33, ikipungua kutoka asilimia 8.36 mwezi uliopita, wakati riba za amana za wateja wakubwa (*negotiated deposit rates*) ziliongezeka kidogo hadi asilimia 11.74 kutoka asilimia 11.66. Kutokana na mwenendo huu, wigo kati ya riba za mikopo na amana za muda mfupi unaopimwa kwa tofauti kati ya riba ya mikopo ya

mwaka mmoja na riba ya amana za wateja katika kipindi cha mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 5.79, ikilinganishwa na asilimia 5.88 mwezi Desemba 2025 (Jedwali 2.3.1).

**Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa Benki za Biashara**

Asilimia

| | Des-24 | Mac-25 | Jun-25 | Sep-25 | Nov-25 | Des-25 | Jan-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.84 | 2.86 | 2.90 | 2.92 | 2.88 | 3.02 | 2.94 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.71 | 15.50 | 15.23 | 15.18 | 15.27 | 15.24 | 15.07 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.74 | 15.83 | 15.69 | 15.52 | 15.53 | 15.46 | 15.49 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.83 | 12.94 | 12.68 | 12.84 | 12.61 | 12.38 | 12.25 |
| Riba za amana -jumla | 8.33 | 8.00 | 8.74 | 8.50 | 8.54 | 8.36 | 8.33 |
| Riba za amana (miezi 12) | 9.62 | 8.14 | 9.79 | 9.84 | 10.02 | 9.58 | 9.70 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 10.39 | 10.35 | 11.21 | 11.05 | 11.67 | 11.66 | 11.74 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 6.12 | 7.69 | 5.90 | 5.69 | 5.51 | 5.88 | 5.79 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.4 Masoko ya Fedha

### Soko la dhamana za Serikali

Katika mwezi Januari 2026, Benki iliendesha minada miwili ya dhamana za Serikali za muda mfupi (*Treasury bills*) yenye thamani ya shilingi bilioni 390.9. Katika kiasi hicho, shilingi bilioni 152 zilielekezwa kugharamia bajeti ya Serikali, huku kiasi kilichobaki kilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa sera ya fedha. Sambamba na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika mfumo wa uchumi, minada hiyo ilipokea zabuni zaidi ya kiwango kilichotangazwa (*oversubscription*), zenye thamani ya shilingi bilioni 514.2, ambapo katika hizo shilingi bilioni 342.2 zilikubaliwa. Wastani wa riba za dhamana za Serikali zilikuwa asilimia 5.89, ikilinganishwa na asilimia 5.87 mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.4.1).

**Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Aidha, Benki Kuu iliendesha mnada wa hati fungani ya miaka 10, wenye thamani ya shilingi bilioni 144.6. Vilevile, mnada huo ulipokea zabuni zaidi ya kilichotangazwa yenye thamani ya shilingi bilioni 194.1, ambapo shilingi bilioni 118.9 zilikubaliwa. Wastani wa riba ya hati fungani (*weighted average yield*) ulipungua hadi asilimia 11.30, ikiashiria kupungua kwa gharama za ukopaji wa Serikali na kuendelea kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika soko la ndani la dhamana za Serikali.

### Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya mabenki liliendelea kufanya kazi kwa ufanisi mwezi Januari 2026, likiwezesha usambazaji wa ukwasi wa shilingi baina ya mabenki. Jumla ya mauzo katika soko hilo yalifikia shilingi bilioni 2,868.9, ikilinganishwa na shilingi bilioni 3,481.9 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia . Mikopo ya siku saba (*7 day tenor*) iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote, ikiwa na asilimia 73.2. Wastani wa riba katika soko la fedha baina ya benki uliongezeka hadi asilimia 6.40 kutoka asilimia 6.29 mwezi Desemba 2025.

**Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Soko la fedha za kigeni

Katika mwezi Januari 2026, ukwasi katika soko la fedha za kigeni baina ya mabenki uliendelea kuwa wa kutosha. Jumla ya mauzo katika soko hili yalipungua hadi dola za Marekani milioni 88.2, kutoka milioni 178.6 mwezi Desemba 2025, (Kielelezo 2.4.3). Benki Kuu ilishiriki katika soko kwa mujibu wa sera ya kushiriki katika soko la fedha za kigeni kwa kuuza dola za Marekani milioni 58, kwa lengo hasa la kukabiliana na mabadiliko makubwa ya thamani ya fedha. Kutokana na hali hiyo, shilingi ilishuka thamani dhidi ya dola ya Marekani, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,477.94 kwa dola ya Marekani mwezi Januari 2026, kutoka shilingi 2,452.76 kwa dola moja ya Marekani mwezi Desemba 2025. Kwa ulinganifu wa mwaka hadi mwaka, shilingi ilishuka thamani kwa asilimia 0.97, ikilinganishwa na ongezeko la thamani la asilimia 2.64 iliyorekodiwa mwaka ulioishia Januari 2025.

**Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Makusanyo ya mapato ya ndani mwezi Desemba 2025 yalifikia shilingi bilioni 4,774.6, ikizidi lengo la mwezi husika kwa asilimia 3. Serikali kuu ilikusanya TZS bilioni 4,654.3, juu ya lengo kwa asilimia 3.9, huku mapato yaliyosalia yakitokana na mamlaka za serikali za mitaa kupitia vyanzo vya ndani.

Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 3,802.7, sawa na asilimia 6.5 zaidi ya lengo la mwezi, ikichangiwa na maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shiling bilioni 851.6, chini ya lengo la shiling bilioni 909.3 (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Disemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

Serikali iliendelea kulinganisha matumizi yake na rasilimali zilizopo kwa kusajili matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 3,671.7.Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 2,643.8 zililekezwa kwa matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 1,027.8 kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

**Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Desemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

## 2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) lilifikia dola za Marekani milioni 51,079.8, ambalo ni ongezeko la asilimia 0.1 kutoka mwezi Desemba 2025. Kati ya kiasi hiki, asilimia 70 ilikuwa ni deni la nje (Kiambatisho, Jedwali A10).

### Deni la Nje

Deni la nje (linalojumuisha deni la Serikali na la sekta binafsi) liliongezeka kwa asilimia 0.6 kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi na kufikia dola za Marekani milioni 35,750.7 kwa mwezi Januari 2026. Katika kiasi hiki, asilimia 82.6 ilikuwa deni la Serikali na kiasi kilichobakia ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1).

Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Januari 2026 ilikuwa dola za Marekani milioni 122.9, ambapo sehemu kubwa ni ya Serikali Kuu. Dola za Marekani milioni 98.5 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo kati ya hizo, dola za Marekani milioni 81.1 zilitumika kufanya malipo ya deni la msingi.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji ulikuwa sawa na mwezi uliotangulia na kipindi kama hicho cha mwaka 2025. Mashirika ya kifedha ya kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu, yakichangia asilimia 58.2 ya deni lote (Jedwali 2.6.2). Mikopo ya urari wa malipo ya nje na utekelezaji wa bajeti (B*alance of Payment and budget support*) iliongoza kwa matumizi ya mikopo iliyopokelewa, ikifuatiwa na mikopo katika shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola za Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya, Euro (Jedwali 2.6.3 na 2.6.4).

**Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopaji | Jan-25 Kiasi | Jan-25 Mchango (%) | Dis-25[r] Kiasi | Dis-25[r] Mchango (%) | Jan-26[p] Kiasi | Jan-26[p] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | 25,851.7 | 80.7 | 29,323.5 | 82.5 | 29,532.9 | 82.6 |
| Deni ambalo halijalipwa | 25,774.5 | 80.5 | 29,243.5 | 82.3 | 29,452.6 | 82.4 |
| Malimbikizo ya riba | 77.2 | 0.2 | 80.1 | 0.2 | 80.3 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 6,171.0 | 19.3 | 6,201.5 | 17.5 | 6,214.1 | 17.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 5,616.6 | 17.5 | 5,776.7 | 16.3 | 5,770.4 | 16.1 |
| Malimbikizo ya riba | 554.4 | 1.7 | 424.8 | 1.2 | 443.7 | 1.2 |
| Mashirika ya umma | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 32,026.4 | 100.0 | 35,528.8 | 100.0 | 35,750.7 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

**Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopeshaji | Jan-25 Kiasi | Jan-25 Mchango (%) | Dis-25[r] Kiasi | Dis-25[r] Mchango (%) | Jan-26[p] Kiasi | Jan-26[p] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 18,175.6 | 56.8 | 20,630.6 | 58.1 | 20,803.5 | 58.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,144.7 | 56.7 | 20,593.7 | 58.0 | 20,766.2 | 58.1 |
| Malimbikizo ya riba | 30.9 | 0.1 | 37.0 | 0.1 | 37.4 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,277.4 | 4.0 | 1,514.4 | 4.3 | 1,526.9 | 4.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,200.2 | 3.7 | 1,434.3 | 4.0 | 1,446.6 | 4.0 |
| Malimbikizo ya riba | 77.2 | 0.2 | 80.1 | 0.2 | 80.3 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,424.4 | 35.7 | 12,669.0 | 35.7 | 12,702.7 | 35.5 |
| Deni ambalo halijalipwa | 11,067.2 | 34.6 | 12,330.2 | 34.7 | 12,347.8 | 34.5 |
| Malimbikizo ya riba | 357.2 | 1.1 | 338.8 | 1.0 | 354.9 | 1.0 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,149.0 | 3.6 | 714.7 | 2.0 | 717.6 | 2.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 982.7 | 3.1 | 665.7 | 1.9 | 666.2 | 1.9 |
| Malimbikizo ya riba | 166.3 | 0.5 | 49.0 | 0.1 | 51.4 | 0.1 |
| Jumla ya deni la nje | 32,026.4 | 100.0 | 35,528.8 | 100.0 | 35,750.7 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi, kwa Asilimia**

| Shughuli ya uchumi | Jan-25 | Dis-25[r] | Jan-26[p] |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 20.4 | 22.7 | 22.7 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.3 | 21.8 | 21.8 |
| Kilimo | 4.9 | 5.3 | 5.3 |
| Nishati na madini | 12.7 | 12.0 | 11.9 |
| Viwanda | 3.6 | 3.8 | 3.8 |
| Huduma za jamii na elimu | 20.1 | 19.3 | 19.4 |
| Fedha na bima | 4.6 | 3.7 | 3.7 |
| Utalii | 1.6 | 1.8 | 1.8 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 4.9 | 5.0 | 4.9 |
| Mengineyo | 5.7 | 4.7 | 4.8 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali.

**Jedwali 2.7.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa Asilimia**

| Sarafu | Jan-25 | Dis-25[r] | Jan-26[p] |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 67.4 | 66.2 | 66.0 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 16.6 | 17.6 | 17.7 |
| Yuan ya China | 6.4 | 6.4 | 6.5 |
| Sarafu nyinginezo | 9.5 | 9.8 | 9.8 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Hadi mwisho wa mwezi Januari 2026, deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 38,599.6, ambalo ni ongezeko la mwezi la asilimia 1.9 (Kielelezo 2.6.1). Sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali ilibakia kuwa hati fungani, huku benki za biashara na mifuko ya hifadhi za jamii vikiendelea kuwa wadai wakuu kwa asilimia 55.2 ya deni lote (Jedwali 2.6.5 na 2.6.6).

**Kielelezo 2.6.1: Deni la ndani la Serikali kuu**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa.

**Jedwali 2.7.5: Deni la ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo**

Shilingi Bilioni

| | Jan-25 | | Dis-25 | | Jan-26$^{P}$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 28,984.2 | 84.9 | 33,012.5 | 87.1 | 32,972.3 | 85.4 |
| Dhamana za serikali za muda mfi | 2,076.4 | 6.1 | 1,951.9 | 5.2 | 1,821.4 | 4.7 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.5 | 135.7 | 0.4 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mr | 26,720.7 | 78.2 | 30,924.8 | 81.6 | 31,015.1 | 80.4 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 5,170.6 | 15.1 | 4,886.5 | 12.9 | 5,627.3 | 14.6 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 5,152.2 | 15.1 | 4,886.5 | 12.9 | 5,627.2 | 14.6 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 34,154.9 | 100.0 | 37,899.0 | 100.0 | 38,599.6 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

**Jedwali 2.7.6: Deni la ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji**

Shilingi Bilioni

| | Jan-25 | | Dis-25 | | Jan-26$^{P}$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Benki za biashara | 9,816.6 | 28.7 | 10,979.6 | 29.0 | 10,902.5 | 28.5 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 7,112.3 | 20.8 | 6,695.2 | 17.7 | 7,436.0 | 19.4 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 9,094.6 | 26.6 | 10,352.2 | 27.3 | 10,389.5 | 27.1 |
| Kampuni za bima | 1,872.6 | 5.5 | 2,006.1 | 5.3 | 2,005.0 | 5.2 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 476.1 | 1.4 | 737.8 | 1.9 | 737.8 | 1.9 |
| Wengine | 5,782.6 | 16.9 | 7,128.0 | 18.8 | 7,128.9 | 18.6 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 34,154.9 | 100.0 | 37,899.0 | 100.0 | 38,599.6 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na na wawekezaji wasio wakazi

Katika mwezi Januari 2026, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 263.7 kupitia uuzaji wa dhamana za Serikali, ambapo shilingi bilioni 113 ni hati fungani na shilingi bilioni 150.7 ni dhamana za Serikali za muda mfupi (Kielelezo 2.6.2). Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 669.8 kulipia deni la ndani, ambapo kati ya hizi, shilingi bilioni 303.9 zilitumika kulipa deni la msingi na shilingi bilioni 365.9 ni malipo ya riba.

**Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Mfadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuimarika, hali iliyoakisiwa na kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida hadi dola za Marekani milioni 1,927.8 kwa mwaka unaoishia Januari 2026 kutoka dola za Marekani milioni 2,448.5 kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.7.1). Hali hii ilichangiwa zaidi na ongezeko la mauzo ya bidhaa nje, hususan dhahabu, sambamba na mapato yatokanayo na huduma za utalii. Ingawa, uagizaji wa bidhaa uliongezeka katika kipindi hicho, ongezeko hilo lilipunguzwa na kushuka kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 6,295.3 mwishoni mwa mwezi Januari 2026, kutoka dola za Marekani milioni 5,323.6 mwishoni mwa mwezi Januari 2025. Kiwango hicho kilitosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.8 ya makadirio ya uagizaji, na hivyo kubaki juu ya lengo la kitaifa na EAC (Kielelezo 2.7.1).

**Jedwali 2.7.1 Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali**

Dola za Marekani Milioni

| | | | | Mwaka ulioishia Januari | | | Mabadiriko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jan-25 | Des-25 | Jan-26 | 2024 | 2025 | 2026p | ya asilimia |
| Urari wa bidhaa | -460.5 | -403.7 | -411.7 | -6,003.2 | -5,100.4 | -4,287.8 | -15.9 |
| Zilozouzwa nje* | 737.7 | 1,090.5 | 1,082.3 | 7,734.4 | 9,251.4 | 10,795.7 | 16.7 |
| Zilizonunuliwa nje | 1,198.2 | 1,494.2 | 1,493.9 | 13,737.6 | 14,351.8 | 15,083.5 | 5.1 |
| Urari wa huduma | 357.65 | 293.9 | 281.5 | 3,925.0 | 4,070.8 | 4,174.9 | 2.6 |
| Mapato | 583.6 | 586.9 | 586.5 | 6,271.8 | 6,879.1 | 7,376.9 | 7.2 |
| Malipo | 225.9 | 293.0 | 305.0 | 2,346.8 | 2,808.3 | 3,202.0 | 14.0 |
| Urari wa bidhaa na huduma | -102.9 | -109.8 | -130.1 | -2,078.2 | -1,029.5 | -112.9 | -89.0 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,321.3 | 1,677.4 | 1,668.8 | 14,006.2 | 16,130.6 | 18,172.5 | 12.7 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,424.1 | 1,787.3 | 1,798.9 | 16,084.4 | 17,160.1 | 18,285.4 | 6.6 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -170.3 | -178.3 | -193.9 | -1,513.4 | -1,955.8 | -2,093.5 | 7.0 |
| Yaliyoingia | 48.2 | 19.4 | 21.0 | 322.9 | 326.9 | 331.1 | 1.3 |
| Yaliyotoka | 218.5 | 197.7 | 214.9 | 1,836.3 | 2,282.8 | 2,424.7 | 6.2 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 32.8 | 6.8 | 12.7 | 709.4 | 536.8 | 278.6 | -48.1 |
| Iliyoingia | 71.1 | 73.3 | 82.2 | 1,301.2 | 1,145.6 | 877.1 | -23.4 |
| ambapo Serikali | 0.0 | 1.5 | 6.6 | 142.9 | 127.3 | 26.3 | -79.3 |
| Iliyotoka | 38.2 | 66.5 | 69.5 | 591.8 | 608.8 | 598.5 | -1.7 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -240.4 | -281.4 | -311.3 | -2,882.2 | -2,448.5 | -1,927.8 | -21.3 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali
*Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

**Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: LHS Inaashiria skeli ya mhimili wa kushoto; RHS, Inaashiria skeli ya mhimili wa kulia

## Mauzo ya nje

Katika mwaka ulioishia Januari 2026, mauzo ya nje ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 12.7 na kufikia dola za Marekani milioni 18,172.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la mauzo ya nje ya bidhaa pamoja na mapato yatokanayo na shughuli za utalii.

Mauzo ya bidhaa, ambayo yanachangia sehemu kubwa ya mauzo yote ya nje, yaliongezeka kwa asilimia 16.7 hadi dola za Marekani milioni 10,795.7 kutoka dola za Marekani milioni 9,251.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku na kahawa, ambapo kwa pamoja yalichangia wastani wa asilimia 70 ya jumla ya mauzo yote ya nje (Kielelezo 2.7.2). Mauzo ya nje ya dhahabu yaliongezeka kwa asilimia 39.3 hadi dola za Marekani milioni 4,900.7 katika mwaka ulioishia Januari 2026 kutoka dola za Marekani milioni 3,517.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili yalichangiwa zaidi na bei nzuri katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji. Mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kwa asilimia 28.9 hadi dola za Marekani milioni 1,702.7 kutoka dola za Marekani milioni 1,320.5, kulikochangiwa na ongezeka kwa mahitaji nchi jirani.

Mauzo ya nje ya bidhaa asilia yaliongezeka kwa asilimia 6.9 hadi dola za Marekani milioni 1,589.4 katika mwaka ulioishia Januari 2026 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya tumbaku na kahawa sambamba na bei nzuri ya mazao haya katika soko la dunia. Mauzo ya korosho yalipungua kutokana na athari za bei na uzalishaji. Kwa ulinganifu wa mwezi, mauzo ya bidhaa nje yalifikia dola za Marekani milioni 1,082.3 mwezi Januari 2026, kutoka dola za Marekani milioni 737.7 mwezi Januari 2025, yakichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa za viwandani.

**Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Katika kipindi cha mapitio, mapato yatokanayo na mauzo ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 7.2 hadi dola za Marekani milioni 7,376.9 kutoka dola za Marekani milioni 6,879.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, yakichangiwa zaidi na mapato ya shughuli za utalii na usafirishaji. Mapato ya utalii yalifikia dola za Marekani milioni 3,969.6, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,933.7 kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa na ongezeko la watalii kwa asilimia 6.1 hadi kufikia watalii 2,289,867. Wakati huo huo, mapato ya huduma za usafirishaji yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,875.4 kutoka dola za Marekani milioni 2,365 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, yakichangiwa zaidi na ongezeko la mapato ya usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani (Kielelezo 2.7.3). Kwa mwezi, mapato ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 586.5 mwezi Januari 2026, kutoka dola za Marekani milioni 583.6 mwezi Januari 2025.

**Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Ukokotoaji wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

## Uagizaji wa bidhaa na huduma

Uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 18,285.4 katika mwaka ulioishia Januari 2026, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.6 kutoka kiwango kilichorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2025. Ukuaji huu kwa kiasi kikubwa ulitokana na uagizaji mkubwa wa bidhaa za viawandani; huduma za usafirishaji; vyombo vya usafiri, mashine na mitambo; bidhaa mtaji na bidhaa za kati. Hata hivyo, uagizaji wa mafuta ya petroli, unaochangia takribani asilimia 13 ya jumla ya uagizaji wote wa bidhaa, ulipungua hadi dola za Marekani milioni 2,380.1 kutoka dola za Marekani milioni 2,552.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Punguzo hili lilichangiwa na kushuka kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia (Kielelezo 2.7.4). Kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa ulifikia dola za Marekani milioni 1,493.9 mwezi Januari 2026, kutoka dola za Marekani milioni 1,198.2 mwezi Januari 2025.

**Kielelezo 2.7.4: Ulinganifu wa Uagizaji wa bidhaa na huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi p inamaanisha takwimu za awali.

Malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 3,202 katika mwaka ulioishia Januari 2026, ikiwa ni zaidi ya dola za Marekani milioni 2,808.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na malipo ya huduma za usafirishaji, sambamba na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje (Kielelezo 2.7.5). Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi , malipo ya huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 305 mwezi Januari 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 225.9 mwezi Januari 2025.

**Kielelezo 2.7.5: Malipo ya Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo:Ukokotoaji wa Benki kuu ya Tanzania

Tanbihi:Huduma nyingine zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za kifedha, mawasiliano ya simu, kompyuta na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili,huduma za kiserikali,huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

